JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

# CHUO CHA MAJI

## UTARATIBU WA MAHAFALI KWA WAHITIMU-2025

Wahitimu wote wa Chuo cha Maji wanataarifiwa kuwa Mahafali yatafanyika tarehe **27 Novemba, 2025** katika **Ukumbi wa Mlimani City** kuanzia **saa 3:00** asubuhi. Tafadhali zingatieni maelekezo yafuatayo ili kuhakikisha utaratibu mzuri wa siku hiyo:

i. **Fomu ya Kuazima Joho:** Wahitimu wote wanatakiwa kujaza fomu ya kuazima joho inayopatikana katika tovuti ya Chuo. Hakikisha umeambatanisha risiti ya malipo iliyotolewa na **Ofisi ya Uhasibu** kabla ya kuwasilisha fomu.

ii. **Wazazi/Walezi:** Kila mhitimu anaruhusiwa kuingia ukumbini na mzazi au mlezi mmoja tu.

iii. **Muda wa Kuingia:** Wazazi na wahitimu wanatakiwa kufika mapema kwani milango ya kuingia ukumbini itafunguliwa **saa 2:00 asubuhi** na kufungwa **saa 2:50 asubuhi**. Tafadhali zingatieni muda ili kuepuka usumbufu.

iv. **Zingatia Utulivu:** Mara mahafali yatakapoanza hakutakuwa na ruhusa ya kutoka nje ya ukumbi. Mtu yeyote atakayetoka nje kwa dharula hataruhusiwa kurudi ukumbini.

v. **Baada ya wimbo wa Taifa** hakuna mhitimu atakayeruhusiwa kuingia ndani ya ukumbi.

vi. **Ugawaji wa Joho**: Majoho yatagawiwa **tarehe 24** hadi **26 Novemba 2025** kuanzia **saa 4:00 hadi saa 10:00 kamili jioni.** Mwisho wa kurejesha ni tarehe **03 Disemba, 2025 saa 10:00 jioni.**

vii. **Rehearsal:** Kutakuwa na mazoezi ya mahafali (rehearsal) **tarehe 26 Novemba, 2025, saa 8:00 mchana** katika **Ukumbi wa Mlimani City**. Wahitimu wote wanatakiwa kuhudhuria kwa maandalizi mazuri ya siku ya mahafali.

Tafadhali zingatieni maelekezo haya ili kufanya siku ya mahafali yenu kuwa ya mafanikio na kukumbukwa kwa kila mmoja. Karibuni sana na tunatoa pongezi nyingi kwa hatua mliyofikia!

**Ratiba ya Mahafali imeambatanishwa!**

Imetolewa na:
**Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**
**20/11/2025**

# RATIBA YA SHEREHE YA MAHAFALI YA AROBAINI NA TISA

| MUDA | TUKIO | WAHUSIKA | MAHALI |
|---|---|---|---|
| 3:00 Asb | Mgeni Rasmi kuwasili na kusaini Kitabu cha Wageni | Mkuu wa Chuo na Bodi ya Chuo | VIP Lounge-Mlimani City |
| 3:00 Asb | Wahitimu na wageni wote kuwasili ukumbi wa sherehe | Wote | Mlimani City |
| 3:30 Asb | Wahitimu, Wageni wa jukwaa kuu na Wanataaluma kujipanga kwa Maandamano | Wahitimu,Wageni na Watumishi wa Chuo | Mlimani City |
| 4:00 Asb | Maandamano ya Kitaaluma | Viongozi na Wahitimu | Mlimani City |
| 4:20 Asb | Wimbo wa Taifa na Afrika Mashariki | Wote | Mlimani City |
| 4:30 Asb | Dua | Aliyeandaliwa | Mlimani City |
| | Kuundwa kwa Mahafali ya 49 | Mgeni Rasmi | Mlimani City |
| | Utambulisho na Utaratibu wa Mahafali | Mkuu wa Chuo | Mlimani City |
| | Burudani | Jazz Band | Mlimani City |
| | Hotuba ya Mkuu wa Chuo na Kumkaribisha Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Maji | Mkuu wa Chuo | Mlimani City |
| | Hotuba ya Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Maji na kumkaribisha Mgeni Rasmi | Mwenyekiti wa Bodi | Mlimani City |
| | Hotuba ya Mgeni Rasmi | Mgeni Rasmi | Mlimani City |
| | Mgeni Rasmi Kutoa Tuzo kwa Wahitimu Bora | Mgeni Rasmi | Mlimani City |
| | Tuzo maalum **“Karia Awards”** | Mkuu wa Chuo | Mlimani City |
| | Kutunuku Shahada za Uzamili, Shahada, Stashahada na Astashahada kwa Wahitimu wa Chuo cha Maji | Mgeni Rasmi | Mlimani City |
| | Kiapo cha Uzalendo kwa Wahitimu | Mkuu wa Chuo | Mlimani City |
| | Burudani | Wote | Mlimani City |
| 6:15 Mch | Mkuu wa Chuo Kumkaribisha Mgeni Rasmi Kuvunja Mahafali ya 49 | Mkuu wa Chuo | Mlimani City |
| | Wimbo wa Taifa | Wote | Mlimani City |
| 6:45 Mch | Kupiga Picha | MC | Mlimani City |
| 7:00 Mch | Mgeni Rasmi kuondoka Ukumbi wa Mahafali | Mgeni Rasmi, Wote | Mlimani City |
| 7:00 Mch | Hafla fupi | Mgeni Rasmi, Wageni waalikwa na watumishi wote. | Mlimani City |